HEKIMA NI UHURU

2020 Na. 39

JARIDA LA TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

# Mulika

MHARIRI MKUU
Mussa M. Hans

MHARIRI MSAIDIZI
Ramadhani T. Kadallah

ISSN 0856 - 0129
e-ISSN-2546-2202

**MULIKA Na. 39** **2020 (79-95)**

# Uchanganuzi wa Miundo ya Aristotle katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

Richard Wafula, Pamela Ngugi na Sophie Okwena[1]

Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Ikisiri**

Makala haya yanalenga kuweka wazi miundo ya Aristotle katika tamthilia ya *Kinjeketile* (1969). *Kinjeketile* ni tamthilia ya Kiswahili ambayo iliandikwa mwishoni mwa miaka ya 1960 wakati ambapo maigizo mengi yalichukua miundo ya Kimagharibi moja kwa moja. Huu ni wakati ambapo Waingereza walileta drama kwa madhumuni ya kujifurahisha wao wenyewe na kujikumbusha maisha ya kwao. Katika kufanya hivi, waliwatumia Watanzania hasa, watoto wa shule katika kuonesha tamthilia za akina Aristotle. Watanzania waliathiriwa kiasi cha kuweza kujishirikisha kikamilifu katika kutunga tamthilia na kuzionesha. Ebrahim Hussein aliandika *Kinjeketile* akitumia miundo ya kina Aristole, hasa tanzia ya Kigiriki ambayo hasa ndiyo msingi wa sheria za ki-Aristotle. Kutokana na masomo yake, Hussein aliweza kuiga miundo ya Aristotle katika utunzi wake.

## 1.0 Utangulizi

Wataalamu mbalimbali waliochunguza tamthilia ya *Kinjeketile* wamekuwa wakijikita na kuegemea katika wahusika, maudhui na mtindo. Licha ya kwamba watafiti wengi walifanya utafiti kuhusu tamthilia ya *Kinjeketile*, suala la miundo ya Aristotle katika tamthilia hii halijashughulikiwa kwa kina. Hivyo basi, kulikuwa na haja ya kuchunguza matumizi ya miundo ya Aristotle katika tamthilia ya *Kinjeketile*. Azma ya kutaka kubainisha miundo hii ndiyo imechochea matumizi ya Nadharia ya Aristotle kwa lengo la kuziba pengo lililoko. Nadharia hii licha ya kuwa ni ya kifalsafa, ni mwafaka katika kuchunguza na kudhihirisha miundo ya Aristotle. Nadharia inajikita katika kuangazia suala la mhusika tanzia na kipengele cha ploti kwa lengo la kutaka kubainisha miundo hii. Akiwa mmoja wa wanafunzi ambao walihudhuria shule za wakoloni na kuingiliana nao kwa namna mbalimbali, Ebrahim Hussein

[1] Baruapepe: sophiejoyedwin@gmail.com

aliweza kuiga miundo yao ya utunzi (Mlama, 1985) na kufikia mwishoni mwa miaka ya 1960 alifanikiwa kutunga tamthilia aliyoiita *Kinjeketile*. Kuishi kwake pamoja na kuingiliana na tamaduni tofauti, kumemfanya kuchukua vipengele vya tamaduni hizo na kuvifanya kuwa vipengele muhimu katika maisha yake na katika kazi zake za kiubunifu (Fiebach, 1997). Zaidi ya hayo, mwandishi huyu hajajifunga katika utambulisho mahususi. Hivyo, Hussein anashirikisha miundo ya kidrama ambayo ilichimbuka kutokana na usomaji wa maandishi tofautitofauti. Katika makala haya mwandishi anakusudia kuchanganua miundo ya ki-Aristotle iliyotumiwa na mwandishi huyu na ambayo inajitokeza katika tamthilia yake ya *Kinjeketile*. Uchanganuzi wa vipengele hivyo umeongozwa na mihimili mahususi ya Nadharia ya Maigizo iliyoasisiwa na Aristotle hususan mhusika tanzia na ploti.

## 2.1 Dhana ya Mhusika Tanzia

Tanzia ni usanii unaohusu kazi ya kifasihi ambayo inaishia kwa anguko la mhusika nguli kutokana na dosari fulani aliyofanya. Nayo ploti ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayoijenga tamthilia, na namna matukio hayo yanavyosababishana. Vipengele hivi viwili vimetumika kama dira katika kupambanua athari ya miundo ya ki-Aristotle katika tamthilia ya Kiswahili.

Katika muktadha wa tamthilia, tanzia huchukuliwa kuwa ni maigizo ya matukio yenye ujumbe mzito yanayowasilishwa kwa lugha inayonawiri ili yazindue hofu na huruma na hatimaye maigizo hayo yalipue hisia za ndani kutoka katika nafsi za hadhira (Gill, 1989). Gill anaendelea kusema kwamba aina hii ya tamthilia huwa na suala, matendo na malengo ya dhati. Waaidha, tanzia ni usanii unaohusu kazi ya kifasihi ambayo inaishia kwa anguko la mhusika nguli kutokana na dosari fulani aliyofanya. Kwa mujibu wa Aristotle, tanzia ni matendo yenye ujumbe mzito yanayoelezwa na kuwasilishwa kwa lugha inayovutia ili yaweze kusababisha hofu na huruma kwa hadhira na hatimaye yalipue hisia za ndani katika nafsi yao (Daiches, 1981). Tamthilia zinazotumia mhusika tanzia ni kazi ya kifasihi zenye usanii uoneshao anguko la mtu ambaye kimsingi ni mwema, shujaa au mbabe kutokana na kosa la kufisha au kutokana na uamuzi mbaya ambao matokeo yake ni mateso (Mutembei, 2005).

## 2.2 Dhana ya Ploti

Ploti ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayoijenga tamthilia, na namna matukio hayo yanavyosababishana (Njogu na Chimerah, 2011). Pia, ploti ni msuko wa matukio hadithini au mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo

vinavyozuana, kusababishana na kuelekezana kwenye suluhisho fulani (Njogu na Chimerah ,2011). Ploti ndiyo moyo wa tanzia kwa sababu matukio makuu ambayo kwayo hadhira hudhihirisha hisia zake ni matendo katika ploti (Aristotle, 1965). Wafula (2003) anasema kwamba jambo analosisitiza Aristotle ni umuhimu wa ploti katika uundaji wa kazi ya sanaa.

## 3.1 Muundo wa Ki-Aristotle katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

Sanaa ya Aristotle ni ile inayozua huruma kwa kumchora binadamu ambaye amesakamwa na mikasa ya kibinafsi (Aristotle, 1965). Kulingana na maoni ya Aristotle, thieta ni chombo cha kufundisha ambacho kinawapa watu nafasi kuchunguza matokeo ya matendo mabaya bila wao kushiriki katika maovu hayo. Kwa hiyo, Aristotle aliona kuwa fasihi ni sanaa inayoiga mazingira yanayomzunguka mtu na hali hii ya kuiga ndiyo huifanya fasihi kutukuka (Wafula, 2003).

Aristotle anasema kwamba lengo la tanzia ni kuwaingiza watazamaji hisia za woga kutokana na yanayompata mhusika mkuu, ambayo yanasababisha anguko lake. Aidha, Aristotle anaona tanzia kama 'mwigo' au 'uigaji' wa tendo ambalo lina udhati, ukamilifu, ubora na ukuu fulani. Hii ina maana kwamba sanaa huiga hali asilia inayomzunguka mtu. Aristotle anaona tanzia kuwa tamthilia yenye huzuni ambayo inagusa hisia za watazamaji kiasi cha kuwaogopesha na kumwonea huruma mhusika mkuu ambaye hupata janga (Mahenge, 2016).

Waingereza walileta drama kwa madhumuni ya kujifurahisha wao wenyewe na kujikumbusha maisha ya kwao wakiwa Afrika. Katika kufanya hivi, walitumia Watanzania hasa, watoto wa shule katika kuonesha tamthilia za akina Shakespeare na Aristotle (Mlama, 2005). Watanzania waliathiriwa kiasi cha kuweza kujishirikisha kikamilifu katika kutunga tamthilia na kuzionesha. Kwanza, Watanzania waliendeleza tamthilia hizohizo za kina Aristotle na Shakespeare lakini baadaye walitunga zao wenyewe ambazo zilihusu maisha katika jamii ya Tanzania. Kutokana na masomo yake, Hussein aliweza kuiga miundo ya Aristotle katika utunzi wake. Tamthilia ya *Kinjeketile* (1969) ambayo ilitungwa wakati huu inadhihirisha vipengele kadha wa kadha vya ki-Aristotle, hususan vipengele vya mhusika tanzia na ploti.

### 3.1.1 Aristotle na Dhana ya Mhusika Tanzia

Tanzia ni aina ya tamthilia yenye uzito unaodhihirika kihisia na huwa na suala na matendo dhati (Gill, 1989). Tanzia ilianza kwenye miviga ya kidini katika Ugiriki ya Kale ikihusishwa na Dionisius (Thomson, 1980). Dionisius alikuwa mungu wa mvinyo ambaye alifanyiwa sherehe za matambiko zilizonuiwa

kumwabudu. Gill (1989) anadokeza kwamba Aristotle aliona tanzia kama 'mwigo' au 'uigaji' wa tendo ambalo lina udhati, ukamilifu, ubora na ukuu fulani (Daiches, 1981).

Lengo la tanzia ni kuwaingizia watazamaji hisia za woga kutokana na yanayompata mhusika mkuu, ambayo yanasababisha anguko lake (Mahenge, 2016). Kwamba tanzia hutumika kuonesha kuanguka au kushindwa kwa mhusika maarufu, mbabe au shujaa. Gill (1989) anafafanua kwamba kulingana na Aristotle tanzia ina sifa zifuatazo:

i. Nguli au mhusika tanzia huwa mtu mashuhuri.
ii. Tanzia sharti iwe na ujumbe mzito.
iii. Kuna usumbufu na mateso kwa nguli.
iv. Kuanguka kwa nguli kusikoepukika.
v. Kiburi kinachomsukuma nguli na kosa la kutofanya uamuzi wa busara.
vi. Kuna taharuki na kejeli.
vii. Kuhusika kwa hadhira na hisia zao mwishoni mwa mchezo.
viii. Utambuzi unaotokana na tanzia.

### 3.1.1.1 Mhusika Tanzia Huwa Mtu Mashuhuri

Kwa mujibu wa Aristotle, shujaa wa tanzia sharti awe mashuhuri, mbabe au atokaye katika tabaka la juu (Gill, 1989). Uchunguzi wetu umeonesha kuwa tamthilia ya *Kinjeketile* inaonesha mambo yaliyosababisha mgogoro wa vita vya Maji Maji na matokeo ya vita hivyo nchini Tanganyika kupitia kwa mhusika nguli Kinjeketile. Mjerumani aliingia nchini humu na kutekeleza utawala wake. Alikuwa akiwatendea wananchi unyama, hali ambayo ilichochea vita vya Maji Maji. Kinjeketile ndiye aliyeleta dhana ya maji kama njia ya kuunganisha makabila ambayo yalikuwa na uhasama. Kwa mfano, umaarufu wake unaonekana kupitia maelezo ya Kitunda anayesema:

**Mfano 1**

> **Kitunda:** Wewe umeleta maji. Wewe umewakutanisha watu wote. Wewe umewafanya watu wakuamini, sasa wapo chini ya madalaka yako....Wamekufuata wewe. Wamekufuata kwa sababu wanakuamini...(uk. 26)

Kulingana na muktadha wa maelezo hapo juu, Kinjeketile anafahamika kote. Anawaamuru watu kueneza nywiywila kusini, kaskazini, mashariki na magharibi. Kitendo hiki kilimfanya Kinjeketile kujulikana kote na kuwa mtu mashuhuri. Makabila yote yalimwamini Kinjeketile na kuungana kwa lengo la kumfukuza Mjerumani. Mwanzoni mwa tamthilia ya *Kinjeketile*, Kinjeketile

anasawiriwa kama mheshimiwa na mtukufu. Tanzia kwa kawaida hujikita katika mhusika mmoja. Mtu mwenye sifa zilizofana na hushikilia nafasi ya juu katika jamii (Gill, 1989: 191).

### 3.1.1.2 Ujumbe Mzito

Ujumbe mzito ni miongoni mwa vipashio vya kisanaa vinavyojenga tamthilia ya kitanzia. Ujumbe huo husheheni maudhui ambayo yanaibua hofu na huruma na hatimaye kulipua hisia za ndani kutoka katika nafsi ya hadhira (Gill, 1989). Tanzia sharti iwe na ujumbe mzito unaogusa hisia za watazamaji (Aristotle, 1965). Ujumbe mzito katika tamthilia ya *Kinjeketile* ni suala la ukombozi kutokana na minyororo ya ukoloni. Ukombozi ambao unaishia katika vifo na umwagikaji wa damu. Nchi ya Tanganyika imekumbwa na mateso ambayo yameletwa na mkoloni ambaye anamdhulumu Mwafrika. Ukatili wa utawala wa Kijerumani unadhihirika wazi hasa tukizingatia kuwa wananchi wanalimishwa kwa nguvu mashambani mwa Mjerumani na hawalipwi chochote kwa jasho lao. Huu ni mfano wa utawala ambamo mtawala anajifikiria mwenyewe tu, asijali mtawaliwa atakula nini. Wananchi wanakabiliwa na shida ya njaa. Wanawake wanahangaika huku na huku wakitafuta kitakachowaokoa. Wanalazimika kula hata mizizi yenye sumu. Mtawala na mtawaliwa wanaendelea kuishi pamoja lakini mtawaliwa hakai tu bali anatafuta mbinu ya kumwondoa mkoloni. Mikutano ya siri inafanywa kwa lengo la kumfukuza Mjerumani ili Waafrika wapate uhuru. Mjerumani anazo silaha na nguvu. Hata hivyo, Mwafrika anajipa moyo kwamba umoja wao utamwondoa Mjerumani. Watu wataendelea kufa njaa hadi lini? Mambo sasa yanafikia hatua ambapo watu wengine wanaona afadhali kufa kuliko kukaa hivi. Haya yanabainika katika mazungumzo kati ya Mkichi na Kitunda kama ifuatavyo:

**Mfano 2**

**Mkichi**: Jambo la kwanza ni kupigana-vita

**Kitunda**: …Tuungane alafu tufanye vita. Watu kidogo kama sisi tutamalizwa mala moja. Nimesikia habali ya bunduki kubwa inayomwaga lisasi kama nchanga.

**Mkichi:** Kwa nini unasita katika shauri hili la vita?

**Kitunda**: Vifo vya watu-maelfu kwa maelfu ya watu… (kur. 6-7)

Kulingana na dondoo, linalojadiliwa hapo juu ni suala zito ambalo linahusisha umwagikaji wa damu. Waafrika walipoanza vita, watu wengi waliuawa. Kitunda anatumika kama msimulizi kuelezea yaliyojiri vitani kama inavyoonekana hapa chini:

**Mfano 3**

**Kitunda:** (*kwa waliohudhiria*) Hivi ndivyo tulivyofikilia. Lakini tulikosa.

Ngulumayo na watu wake wakaanza kuvamia boma bila kuchukua nazali yoyote. Tulifikilia kuwa habali ya bunduki kubwa yote ilikuwa uwongo…(uk. 45)

Belfiore (1992) anadokeza kwamba kwa mujibu wa Aristotle, tendo hilo zito sharti liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni na woga. Katika dondoo hapo juu, Kitunda anasimulia kwa huzuni jinsi maelfu ya watu walivyouawa katika vita. Huu ni ujumbe mzito ambao umesheheni maudhui yanayoibua hofu na huruma katika nyoyo za hadhira, na hatimaye kuifanya tamthilia husika kuwa ya kitanzia.

### 3.1.1.3 Usumbufu na Mateso kwa Nguli

Mateso ya mhusika tanzia huwa yanakithiri, yaani mhusika tanzia hateseki tu, bali huteseka kupita kiasi. Waaidha, mhusika tanzia hujikuta katika ushindwaji, mivutano na janga. Katika tanzia, mhusika mkuu hukumbwa na misukosuko fulani, matatizo au dhiki na wakati mwingine huishia kwa kifo (Aristotle, 1965). Mawazo ya Aristotle (1965) yanatiwa nguvu zaidi na maelezo ya Gill (1989) ambaye anadokeza kwamba mhusika tanzia sharti ateseke kwa matendo yake na labda afe. Mawazo ya Aristotle yanadhihirika katika *Kinjeketile* ambapo Kinjeketile ambaye ni mhusika tanzia anateswa sana. Hapa chini ni ithibati ya maelezo haya:

*Ndani ya ngome. Kinjeketile, uso na mwili wake una damu tupu. Inaonesha kapigwa sana. Wanapoingia kina Kitunda, Kinjeketile hana fahamu. Watu wamemkaribia Kinjeketile na kumtambua… (uk. 46)*

Kutokana na dondoo hapo juu, Kinjeketile ambaye ni mhusika tanzia anapitia mateso hayo lakini hafi au labda anakufa baadaye kulingana na maelezo ya Ebrahim Hussein. Kinjeketile anakamatwa, na kutiwa ndani. Anachapwa hadi anapoteza fahamu. Aidha, anacharazwa kwa viboko hadi mwili wake pamoja na uso wake vinajaa damu tupu. Kinjeketile anapitia mateso mengi ambayo yamekithiri wakati anapokamatwa na kuzuiliwa.

### 3.1.1.4 Kuanguka kwa Nguli Kusikoepukika

Kuanguka kwa nguli mara nyingi hakuepukiki. Inakuwa uchungu mkubwa kwa hadhira kushuhudia matukio ambayo inayaona kuwa hayakwepeki. Katika tanzia anguko la shujaa huja kutokana na uamuzi wake mbaya au kosa lake mwenyewe (Mutembei, 2005). Baada ya Kinjeketile kugundua kwamba alipotoka ndani ya maji aliwaambia watu kwamba Mjerumani akitoka

watatawaliwa na Seyyid Said, alianza kuwa na wasiwasi. Aliona kwamba amedanganywa na akaanza kumshuku Hongo, mungu wa Wamatumbi.
Aidha, Kinjeketile alianza kuwa na wasiwasi kuhusu dhana ya maji ambayo alikuwa amewahakikishia watu kwamba kuna nguvu katika maji. Katika hatua hii, Kinjeketile hangeweza kuwaambia watu ambao walikuwa tayari kupigana kwamba ana wasiwasi ndani yake kumhusu Hongo. Wala hangeweza kuwaambia kwamba huenda, "maji" aliyowaahidi yasiwe na nguvu. Haya yanadhihirika hapa chini:

**Mfano 4**

**Kinjeketile**: Chukueni na aminini maji ya maisha. Chukueni maji ya nguvu. Chukueni na aminini maji yanayotia ushujaa... (uk.18)

Kinjeketile anapogundua kwamba alisema kuwa baada ya Mjerumani kuondoka watatawaliwa na Seyyid Said, uso wake unabadilika na kuhisi kwamba Hongo aliyekuwa amemwamini anamchezea kama inavyodhihirika hapa chini:

**Mfano 5**

**Kinjeketile:** Nimedanganywa. Wameniuwa, nimejiuwa mimi mwenyewe. Ilikuwa ndoto nikiota! Apana! Wamenidanganya (uk. 20)

Aidha, Kinjeketile anaona kwamba Hongo amemsaliti na fikra zake zinaanza kubadilika kumhusu Hongo anaposema hivi:

**Kinjeketile**: ...Kwa nini Hongo anataka kutuuza sisi watoto wake kwa mabwana wengine? Haya ni maswali magumu. Hakuna anayeweza kujibu ila Hongo. Nikienda kwake pengine ndiye yule anayetaka kutuuza sisi kwa Seyyid Said...Lazima nipate wahyi kutoka kwa Mungu (uk. 27)

Kuanguka kwa shujaa kumesababishwa na makosa anayoyafanya yeye mwenyewe na pia wakati mwingine kunatokea kwa sababu tu ni lazima kutokee. Kwa mujibu wa Aristotle (1965) hakuna kosa la bahati mbaya, kila mkasa wa kufisha ni matokeo ya maamuzi mabaya au kosa fulani. Uneni wa Kinjeketile hapo juu haungemruhusu kuwaeleza watu ukweli kwamba amedanganywa na kwamba maji hayana nguvu; badala yake aliamua kujinyamazia. Hili ni anguko ambalo Kinjeketile hangeweza kuliepuka. Kinjeketile anasema, " ...Ikiwa huyu Sayyid Said anaweza kutumiliki akili zetu bila sisi wenyewe kujua, akaweza kututumia bila kujua, basi yeye ni adui mkubwa kuliko Njerumani...Tutapigana na tutashinda. Ngojea" (uk. 27).

Mvutano kati ya uhuru na udhibiti bila shaka upo katika tanzia. Aidha, kuna mivutano baina ya ukweli kwamba nguli hufanya maamuzi yaliyo huru na hisia, kwamba kuna nguvu zinazoonekana ambazo zinamdhibiti. Hata hivyo, suala la mvutano haliwezi kusuluhishwa kiasi ambacho nguli yuko huru au amedhibitiwa sawia na kuanguka kwake.

Pia, wakati nguli anapoanguka hata lugha yake hubadilika. Mwanzo kabla ya kuanguka kwake, huwa anaitawala lugha yake lakini baadaye mazungumzo huwa hayana muwala yaani, anaweza kuwa anasitasita (Gill, 1989). Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kinjeketile*, Kinjeketile anapotoka ndani ya maji anaitawala lugha yaani anaongea lugha sanifu. Anasema kwa maghani kwa ustadi wa hali ya juu kama inavyodhihirika hapa chini:

**Mfano 6**
**Kinjeketile**: Jua limetoka
Tazameni jua limetoka
Linaangaza na kuzagaza nuru yake…(uk. 14)

Wakati ambapo Kinjeketile anagundua kuwa amesema kwamba baada ya Mjerumani kuondoka Seyyid Said ndiye atawatawala, anaanza kuwa na wasiwasi na lugha yake inabadilika. "…Na sisi tutakuwa watu wa Seyyid Said" (uk. 15). Kuwa watu wa Seyyid Said ni kuingiwa na ukoloni mamboleo ambao una hatari kubwa kuliko ukoloni wenyewe….Kinjeketile anasema hivi: "Ikiwa huyu Seyyid Said anaweza kutumiliki akili zetu bila sisi wenyewe kujua, akaweza kututumia bila kujua, basi yeye ni adui mkubwa kuliko Njerumani. Anaweza kututawala hali yupo nje ya nchi" (uk.27).

Kulingana na Aristotle, kuna sababu kadha ambazo husababisha anguko la nguli katika tanzia (Gill, 1989): Kwanza, nguli ana kasoro kubwa, na pili, nguli huenda kinyume na maadili ya kijamii. Wazo la nguli kuwa na kasoro ina maana kwamba ana udhaifu ambao akiwa ameshinikizwa husababisha maafa. Aidha, wazo la kuenda kinyume cha maadili ya kijamii ni kwamba nguli ana kiburi cha kujiamini kilichovuka mipaka. Haya huweza kuonekana wakati nguli anapoamua kukiuka kanuni za kimsingi za maisha zinazohusu maadili ya dini. Hapa, nguli huamini kwamba yu sahihi na kwamba jukumu lake ni muhimu kuliko uadilifu.

#### 3.1.1.5 Kiburi Kinachomsukuma Nguli na Kosa la Kutofanya Uamuzi wa Busara

Mhusika tanzia ana kiburi au fahari inayomsukuma hadi mwisho wa maisha yake na fahari hiyo wakati mwingine huwa ni 'kiburi' ambacho humshurutisha

mhusika kujisaka na kuishia katika hali ya kuhuzunisha (Wafula na Njogu, 2013). Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kinjeketile,* kiburi hiki kinamfanya Kinjeketile kuvumilia mateso, kukataa kukanusha 'maji', kwani angesema watu kutoka sehemu za kusini na kaskazini, wangeacha kupigana, wangekosa ari. Kinjeketile anataka kujua iwapo, 'kupigania nchi ni makosa'. Anavumilia mateso akijua kwamba, "watoto wetu watawaambia watoto wao neno hilo...Wajukuu wetu watasikia. Siku moja neno hilo halitakuwa ndoto, bali ukweli" (uk. 49).

Kiburi humzindua mhusika kutetea imani na fahari yake licha ya kwamba mambo haya yatasababisha kifo chake. Kutokana na ukweli wa maoni hapo juu, ni dhahiri kwamba kupitia kiburi cha Kinjeketile, Tanzania iko huru, kwani mgogoro ulioanzishwa na mtu huyu haukumalizika watu waliposhindwa. Watu hawawezi kunyimwa uhuru wao daima. Ingawa mwanzo hawatafaulu, hatimaye lazima watafanikiwa katika kujikomboa kwenye hali ya unyonge. Kiongozi mmoja akiondoka, au akiondoshwa, baada ya muda huja mwingine wa kuendeleza mbele 'neno' la uhuru. Leo hii neno hilo si ndoto tena.

### 3.1.1.6 Taharuki na Kejeli

Migogoro inayotangulizwa na kukuzwa katika tamthilia inaendelezwa kwa kutumia vipashio mbalimbali vya kisanaa hususan taharuki na kejeli. Taharuki inampa mtazamaji au msomaji ilhamu ya kujiuliza kuhusu yatakayotokea baadaye (Morgan, 1964). Matukio yanayojiri kinyume na matarajio ya wahusika na wakati mwingine kinyume na matarajio ya watazamaji wa tamthilia huzalisha hali ya kejeli. Ebrahim Hussein katika utunzi wa *Kinjeketile,* anamchora mhusika mkuu ambaye usemi wake ni kinyume na matarajio ya watazamaji. Kinjeketile anapotoka ndani ya maji alikokaa kwa muda wa siku moja anasema hivi:

**Mfano 7**

**Kinjeketile:** Baada ya kuwa kitu kimoja, baada ya kuwa mwili mmoja tutakuwa watu wa Seyyid Said. Udongo mwekundu atapigwa na atatolewa nchini. Na sisi tutakuwa watu wa Seyyid Said... (uk. 15)

Kitunda anamwarifu Kinjeketile kwamba, alipotoka majini alisema kuwa watu wote watakuwa chini ya Seyyid Said. Huu ndio wakati ambapo Kinjeketile anaona kwamba amedanganywa, ameuawa na ni kama alikuwa ndotoni. Habari inamweka msomaji katika hali ya taharuki. Msomaji anabaki akijiuliza

maswali chungu nzima. Kutapiganwa vita kweli? Waafrika watashinda au watashindwa? Maji yalikuwa ukweli au uongo? Kwa upande mwingine, matamshi ya Kinjeketile kwamba watu watakuwa chini ya Seyyid Said, ni kejeli kwa wasomaji kwa sababu wanafikiria kwamba Mjerumani akiondoka watakuwa huru. Hii ndiyo sababu ambayo imemfanya Kitunda kutaka kujua zaidi kuhusu huyo Seyyid Said. Hali hii inakuwa kinyume cha matarajio ya msomaji au mtazamaji kama tunavyoona hapa chini:

**Mfano 8**

**Kitunda:** Kama ulivyokuwa ukisema wewe unapohutubia, na unapofundisha, unasema lugha ngeni-kama Kialabualabu.

**Kinjeketile:** Mimi?

**Kitunda:** Wewe.

**Kitunda:** Ulisema kuwa sisi sote tutakuwa watu wa Seyyid Said.

**Kinjeketile:** Mimi? Nilieze nilivyosema. Kila kitu tafazali.

**Kitunda:** Ulisema kuwa lazima tuwe kitu kimoja....Ukasema tukisha shinda tutakuwa watu wa Seyyid Said.

**Kinjeketile:** Nimedanganywa. Wameniuwa, nimejiuwa mimi mwenyewe (uk. 20).

Inawezekana kuwa Mjerumani akiondoka baadaye Watanganyika watakuwa chini ya mtawala mwingine? Huku kutakuwa kujitawala au kutawaliwa tena? Hayo maswali yote yanakuwa kama kejeli kwa wasomaji. Huenda ikawa Kinjeketile hakuingiwa na Hongo wala kukaa majini kwa muda wa siku moja? Hayo maswali yote yanaelekea kwenye kitu kimoja yaani taharuki ambayo imewakumba Watanganyika kama inavyodhihirika hapa chini:

**Mfano 9**

**Kinjeketile:** Unajuaje kama huyu ni Hongo, au si Hongo. Ikiwa pepo huyu ni wetu, kwa nini anasema tutakuwa watoto wa Seyyid Said baadaye? Kwa nini?... (uk. 26-27)

Katika dondoo hapo juu, Kinjeketile mwenyewe ana wasiwasi kuhusu usemi wake wa kuwa na nguvu katika maji. Ni kejeli kwamba Kinjeketile ambaye ameleta dhana ya maji naye pia anakuwa na wasiwasi kuhusu Hongo ambaye alimpa dhana ya maji. Kitunda anapomwarifu Kinjeketile kuhusu usemi wake baada ya kutoka ndani ya maji kwamba watatawaliwa na Seyyid Saidi, anaanza kumshuku Hongo.

### 3.1.1.7 Kuhusika kwa Hadhira na Hisia zao Mwishoni mwa Mchezo

Katika tanzia hadhira hualikwa kuelewa kinachomkumba nguli, si kama mtazamaji aliye kando bali huhisi anavyohisi nguli (Gill, 1989). Hisia zinazoibuliwa ni za huruma kwa kuwa vitu vibaya vinatendeka, na ambavyo hadhira inaviona kuwa ni lazima vitokee lakini kamwe haina uwezo wa kuvizuia. Hadhira hushuhudia kudhoofika kwa mhusika nguli na kumhurumia ingawa inafahamu kuwa haina uwezo wowote wa kubadilisha matukio hayo. Katika hatua hii, hata wahusika wengine pia hawana uwezo wowote wa kubadilisha matukio hayo. Hali hii huweza kuifanya hadhira kupiga kelele kwa kutamauka kwa jinsi mhusika mhasiriwa alivyopotoka. Hadhira huishia kumhurumia mhusika anayeteseka.

Tendo la tanzia sharti liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni au kihoro pamoja na kuwa na uwezo wa kuzitakasa hisia za woga au huzuni katika kile kilichojulikana kama mtakasohisia. Kwa mujibu wa Aristotle (katika Thomson, 1980), mtakasohisia ni hisia anazopata mtazamaji ambaye amesoma na kuitazama tanzia (taz. pia Wamitila, 2002). Hisia hizi hazilengi kumvunja mtu bali zinadhamiria kuleta faraja au tulizo fulani linalotokana na kuzitakasa hisia za ndani. Madhumuni ya mtakasohisia ni kumfanya mtazamaji kujihisi pamoja na binadamu wengine. Waaidha, kuna uwezekano wa hadhira kuhisi hasara kwa vile tanzia huonesha kuanguka na usumbufu kupita kiasi kwa mtu muhimu na mashuhuri. Dondoo hapa chini linathibitisha maelezo haya:

> **Mfano 10**
> **Kitunda:** Kwa nini kapigwa nanna hii?
> **Askari**: Daudi mtie maji huyu.
> (*Daudi anamwagia maji Kinjeketile)*
> **Askari:** Amekataa?
> *Kitunda amepigwa bumbuazi...*
> *Anapigwa tena. Anaanguka pole pole...hana nguvu)*....(uk. 47)

Katika dondoo hapo juu, Kitunda anaathirika sana na mateso ambayo Kinjeketile anayapitia. Kwamba mtu mashuhuri ameishia kuwa si chochote katika jamii. Nguvu na uwezo wa Kinjeketile haupo tena. Hali hiyo inamfisha moyo Kitunda,

Hadhira pia inaweza kuingiwa na hofu na huruma. Hadhira huwa na hofu kwa vile inaona kwamba ni jambo litakalomfika yeyote. Hofu ambayo huchipuzwa na tanzia ni ile ya kuogofya. Huruma na hofu inamfanya Kitunda kushangaa sababu ambayo imefanya Kinjeketile kupigwa namna alivyopigwa. Hisia hizi

ambazo huja mwishoni mwa mchezo husababishwa na mateso ambayo mhusika tanzia huyapitia. Hata hivyo, hadhira hutambua kuwa tanzia haihuzunishi. Hadhira haitoki ukumbini na nyoyo zenye huzuni na zilizotamauka, bali hutoka na hisia za msisimko na zenye kutiwa nguvu. Gill (1989) anajaribu kutoa sababu ambazo husababisha hali kama hii kutokea. Anatumia dhana tatu kuelezea hali hii. Dhana hizo ni mtakaso, udhati na heshima ya mwanadamu.

Katika dhana ya udhati, tanzia huikumbusha hadhira kwamba, maisha si mzaha. Haya yote tunayaona licha ya usumbufu uliokithiri alioweza kupitia Kinjeketile anaamini kwamba, Tanganyika itajitawala siku moja. Hatimaye, tanzia huweza kuikumbusha hadhira kuwa binadamu huweza kuwa wa heshima na mwenye thamani. Katika *Kinjeketile* tunaona ushujaa, thamani, moyo usioyumbishwa, upendo na stahamala za mhusika tanzia. Haya yote tunayaona licha ya udhaifu na usumbufu uliokithiri.

### 3.1.1.8 Utambuzi Unaotokana na Tanzia

Utambuzi ndio hufanya tanzia kuwa na nguvu au uwezo zaidi (Aristotle, 1965). Aristotle (1965) anazungumzia utambuzi wa hali ya juu unaotokea katika tanzia. Utambuzi huu hutokana na hali anazopitia mhusika tanzia na pia ushuhuda wanaomtolea wahusika wengine. Kulingana na Aristotle, mwisho wa tanzia huwa ni utambuzi na ufunuo wa mafundisho (Wafula, 2003). Katika tamthilia ya *Kinjeketile,* watu wanapata funzo kuwa, hawawezi kunyimwa uhuru wao daima. Ingawa mwanzo hawatafaulu, hatimaye sharti watafanikiwa katika kujikomboa kwenye hali ya unyonge. Hii ndiyo sababu inayomfanya Kinjeketile kukataa kukiri kwamba maji yalikuwa uongo. Kiongozi mmoja akiondoshwa au akiondoka, baada ya muda huja mwingine wa kuendeleza mbele 'neno' la uhuru. Maelezo haya yanadhihirika kama ifuatavyo:

**Mfano 11**

**Kinjeketile**: Hapana! Sitasema neno hilo….Neno limezaliwa. Watoto wetu watawaambia watoto wao neno hilo. Wajukuu wetu watalisikia. Siku moja neno hilo halitakuwa ndoto, bali ukweli. (uk. 49)

Kinjeketile anaamini kwamba, harakati hizi zitaendelezwa na watoto wao pamoja na wajukuu wao. Huu ndio utambuzi unaotokea katika tanzia. Utambuzi huu hutokana na hali anazopitia mhusika tanzia, na pia ushuhuda anaowatolea wahusika wengine. Hii ndiyo sababu anasema kwamba neno limezaliwa na litakua na kunawiri.

### 3.2 Kipengele cha Ploti

Kulingana na Aristotle, ploti sharti iwe na sehemu tatu: mwanzo, kati na mwisho (Daiches,1981). Mwanzo wa tamthilia una kichocheo. Hili ni tukio linalotegua mtawalia wa matukio yanayofanyika katika tamthilia. Kichocheo huibua matukio ambayo hufululiza taratibu hadi kufikia kwenye suala kuu la kuigizwa na kujadiliwa katika tamthilia. Mwanzo wa tamthilia ya *Kinjeketile* (1969), unaonesha mateso ambayo yanawapata Waafrika. Mjerumani anawafanyisha Waafrika kazi kwa kuwalimisha mashamba. Mkoloni aliingia nchini Tanganyika na kuyavuruga maisha ya wenyeji. Maelezo haya yanapatikana kupitia kwa Bi. Kitunda na Bi. Kinjeketile wanapojadiliana kuhusu mateso wanayoyapitia kama inavyobainika hapa chini:

**Mfano 12**

**Bi Kitunda:** Habali, Bi Kinjeketile?

**Bi Kinjeketile:** Nzuli, nzuli. Salama?

**Bi Kitunda:** Salama tu. Leo watu hawajaludi mpaka sasa. Wamechelewa.

**Bi Kinjeketile:** Shamba la Bwana Kinoo limezidishwa ukubwa sasa. Kila ntu nasikia kapata mahali pakubwa zaidi...(uk. 1).

Katika desturi za Kiafrika, wanaume hushiriki katika kupanda na kulima mashamba. Chakula cha nyumbani hutoka shambani. Lakini Mjerumani alipokuja aliuvuruga utaratibu huu kwa kuwachukua wanaume wote na kuwalazimisha kulima katika shamba lake. Hapa inadhihirika kwamba mtawala anajifikiria mwenyewe tu, bila kujali masilahi ya mtawaliwa. Mzalendo anapanda asipovuna, Mjerumani anavuna asipopanda. Wananchi wanakabiliwa na shida ya njaa. Mtu mgeni amekuja nchini na kuwafanya wenyeji watumwa wake. Katika sehemu hii pia mhusika tanzia amerejelewa na kutajwa. Malalamishi haya ndiyo yanatoa picha ya hali iliyopo, mivutano au migogoro ambayo imeanza kujitokeza kama ifuatavyo:

**Mfano 13**

**Bi Kitunda:** …tulipoona Moshi tukafikili unapika.

**Bi Kinjeketile:** Moshi ule…Kinjeketile huyo anafanya kafala. Kajifungia ndani leo siku ya ngapi sijui.

**Bi Kitunda:** kweli mimi simuoni. Lakini nanna gani yeye anaweza kukaa ndani bila kwenda shambani?...

**Bi Kitunda:** Siku moja nikankuta ntoni peke yake, mimi nilikwenda kalibu akuniona. Alikuwa anafata nto unakotokea. Anatazama maji kama hajayaona.

**Bi Kinjeketile:** Kabadilika sana. Analosema mimi silisikii…(uk. 2)

Matendo ya Kinjeketile ya kujifungia nyumbani na kufanya kafara na kuonekana mtoni akifuata mto unakotokea, yanategua mtawalio wa matukio yanayofanyika katika tamthilia ambayo hufululiza hadi kufikia kwenye suala kuu.

Sehemu ya kati ni ile ambayo hukuza mgogoro na ndiyo huchukua sehemu kubwa sana ya tamthilia. Sehemu ya kati ndipo shujaa anatambulishwa na utata (Belfiore, 1992). Mgogoro huu unakuzwa kwa kuonesha mielekeo tofauti ya wahusika. Katika sehemu hii ama kuna mkweo wa tendo lililioanza na ambalo baada ya muda huelekea kwenye utata au ukinzani kisha kwenye upeo au kilele. Sehemu ya kati inahusu kilele cha juu ambapo misako migumu wanayoifanya inaigizwa. Ni katika sehemu hii ambapo bahati au jaala ya shujaa wa tanzia inatishiwa dhahiri.

Katika tamthilia ya *Kinjeketile,* hii ni sehemu ambapo Kinjeketile ambaye ni shujaa wa tanzia anajitokeza wazi. Kinjeketile anapandwa na Hongo na kukaa ndani ya maji kwa siku moja nzima. Anawaletea watu maji ya kuwafanya wasidhurike kwa risasi. Bahati yake iko katika tishio dhahiri wakati anaanza kushuku yale ambayo alikuwa akiwaeleza watu baada ya kurejea kutoka mtoni. Huu ni wakati ambapo Kitunda anamwambia kwamba yeye Kinjeketile alisema kuwa watakuwa watu wa Seyyid Said. Kinjeketile anaona kwamba Hongo amemdanganya. Ni wakati huu ambapo Kinjeketile anaanza kuogopa kuwaambia watu waende kupigana na Mjerumani. Kitunda mwenyewe anajaribu kuwazuia watu wasiende kwenye vita kwa sababu amekwishakujua ukweli. Neno ambalo Kinjeketile analitoa linakuwa kubwa kumshinda yeye. Watu wako tayari katika vita, huku Kinjeketile akiwa na mgogoro ndani yake kwa sababu ameona kwamba amedanganywa na tayari nywinywila zishafika kila sehemu. Yaani, habari za Vita vya Maji Maji zilikuwa tayari zimevuka mipaka. Vijana walikuwa wamejitokeza tayari kupeleka habari kusini, kaskazini, mashariki na magharibi. Habari za maji zilikuwa zimeenea pote kwamba 'maji' ni dawa na yeyote atakayepigwa risasi hatadhurika.

Sehemu ya kati ya mwisho kulingana na Ferguson (1972) huwa ni kipeo cha mchezo. Katika kipeo, matishio mbalimbali ya ploti huja pamoja na kusuluhishwa. Kipeo siyo mwisho wa mchezo au tamthilia kulingana na Aristotle. Kwa mfano, Wamatumbi, Wazaramo, Wakichi, Wangindo na watu kutoka makabila mbalimbali wameitikia wito na nywinywila za Kinjeketile. Sasa wako tayari kupigana. Kitunda amejaribu kuwazuia wangoje neno la mwisho kutoka kwa Kinjeketile hadi hawezi tena kuwazuia zaidi. Kitunda anaenda kwa Kinjeketile kwa ushauri zaidi. Kinjeketile hana jawabu kwa

sababu hata yeye anahofia maisha ya watu. Kunatokea ubishi kati ya Kinjeketile na Kitunda. Kinjeketile anamwambia Kitunda kwamba, kupigana wapigane lakini wasitegemee maji. Mgogoro huu tunaweza kuuona vyema katika dondoo hii:

**Mfano 14**

**Kitunda:** Wamekufuata wewe. Wamekufuata kwa sababu wanakuamini. Na wewe unawakimbia.

**Kinjeketile:** (*kwa hamaki)* watu hawaniamini mimi. (*Sauti ya kawaida*) Watu Wanaamini maji. Na ulivyosema kuwa uwaambie vita hakuna…

**Kitunda:** Tunao umoja, na watu tupo-wa kutosha-wote tayali kwa vita.

**Kinjeketile:** Kupigana tupigane, lakini tusitegemee maji.

**Kitunda**: (*anamsuta*) Wewe ndiye uliyeleta maji.

**Kinjeketile:** Mimi sikuleta maji, mimi…(kur. 25-26).

Baada ya Kitunda kuchoka kuwasubirisha watu eti wangoje siku moja zaidi, mwishowe, Kinjeketile anawaruhusu watu kwenda kupigana. Watu wengi wanauawa. Huu ndio upeo wa mchezo.

Baada ya kipeo, kuna mwisho au hitimisho ambapo kulingana na Aristotle sharti hali mpya iwepo ambayo inaitwa utatuzi. Mwisho pia unashirikisha mafunzo ambayo hadhira au nguli hupata kutokana na tajriba ngumu ambazo wahusika wamepitia. Huu ndio mwisho wa tamthilia kulingana na Aristotle. Katika *Kinjeketile*, baada ya watu kufa, Kinjeketile anakamatwa na kutiwa ngomeni. Anateswa na askari wa Kijerumani ili akiri kwamba maji yalikuwa uongo lakini Kinjeketile anakataa kukiri kama inavyodhihirika hapa chini:

**Mfano 15**

**Kinjeketile**: …. Ulijaribu nilivyokuambia?

**Kitunda**: Hakuna aliyenisikiliza. Ingekuwa wangefuata….

**Kinjeketile**: (*haraka*) Hakuna majuto. Hakuna majuto. Limefanyika basi. *(Peke yake)*
Neno likintawala ntu badala ya ntu kulitawala neno…(uk. 48)

Kulingana na usemi huu, Kinjeketile amejuta kwa neno lake anapoona kuwa linamwangusha lakini hatasema ukweli juu ya neno hili maana kusema hivyo ni kuwavunja watu moyo.

## 4.0 Hitimisho

Makala haya yametathmini ufasiri na uhakiki wa miundo ya Aristotle katika tamthilia ya *Kinjeketile*. Mihimili ya Nadharia ya ki-Aristotle imetumiwa kudhihirisha wazi ujitokezaji wake katika tamthilia ya *Kinjeketile*. Katika uchanganuzi huu imebainika kwamba Ebrahim Hussein ameshirikisha miundo ya Aristotle katika tamthilia yake. Vipengele vya ki-Aristotle ambavyo ameshirikisha ni pamoja na umashuhuri wa nguli, ujumbe mzito katika tanzia, usumbufu na mateso kwa nguli, kutokwepa kwa anguko la nguli, fahari inayomsukuma nguli, kosa la kutofanya uamuzi wa busara, kuhusika kwa hadhira na hisia zao mwishoni mwa mchezo, utambuzi unaotokana na tanzia na kipengele cha ploti.

## Marejeleo


Aristotle, G. 1940). "Poetics" *In Literary Criticism: Plato to Dryden*. Allan G. (ed). New York: American Book Company.

Aristotle, G. (1965). *ThePoetics*. Harmondsworth: Penguin.

Aristotle, G. (1965). *Introduction to Aristotle*. Dorsch S. (ed). USA: McGraw Hill Education Publishers.

Belfiore, E. (1992). *Tragic Pleasures: Aristotle on Plot and Emotion*. Princeton: Princeton University Press.

Crow, B. and Banfield, C. (1996). *Introduction to Post-Colonial Theatre*. Cambridge: Cambridge University Press.

Daiches, D. (1981). *Critical Approaches to Literature*. London: Longman.

Ferguson, J. (1972). *Aristotle*. New York: Twayne Publisher.

Fiebach, J. (2002). *Ebrahim Hussein's Dramaturgy: a Swahili Multiculturalist's Journeyin Drama Theatre*. The Ohio State University: Indiana University Press.

Hussein E. (1969). *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (2003). "Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle," katika *Makala za Seminaya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 197-205.

Mahenge, E. (2016). *Drama za Kiswahili*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Mlama, P. (2003). "Hali ya Sanaa za Maonyesho Tanzania," katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 186-196.

Mlama, P. (2003)."Utunzi wa Tamthilia katika Mazingira ya Tanzania," katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi waKiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 206- 225.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JKF.

Sengo, T. (1975). "Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii", Katika *Kiswahili*. Juz. Na. 43 (2): 76-78. Dar es Salaam. TUKI.

Sophocles, K. 1947). *Antigone*. Middlesex: Penguin.

Sophocles, K. (1947). *Oedipus the King*. Middlesex: Penguin.

Syambo, B. (1990). *Mwongozo wa Kinjeketile*. Nairobi: Heinmann Kenya Ltd.

Wafula, R. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo* Yake. Nairobi: JKF.

Wafula, R. na Njogu K. (2013). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: JKF.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers

Wamitila, K. (2012). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.